SHULE YA SEKONDARI SEEKE
S.L.P 1021
BARUA PEPE: seekesecondary@gmail.com
MOBILE NO. 0755297239

TAREHE ……

Kumb Na. ……

Jina la mwanafunzi: …….

S.L.P ……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SEEKE ILIYOKO HALMASHAURI YA MJI KAHAMA MKOA WA SHINYANGA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

Shule ya sekondari Seeke ipo umbali wa km 8 mashariki mwa mji wa Kahama mkoa wa shinyanga.

Usafiri unaopatikana kutoka mjini hadi shuleni ni wa bajaji , pikipiki au baiskeli.

Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe 11-01-2021, hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11-01-2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18-01-2021 ndani ya siku saba.

2.**0 MAMBO MUHIMU**

2.1 SARE ZA SHULE:

a) Wasichana;

i) Sketi mbili rangi ya ugoro-udongo mashono ni rindabox(***rinda kubwa nyuma na mbele***) ndefu inayokaribia vifundo vya miguu lakini iruhusu soksi zionekane, kitambaa kimeambatanishwa, hii ni kwa wanafunzi wote hata wale wanaovaa Hijabu, suruali hazitakiwi.

ii) Mashati mawili meupe***(blauzi***) tetroni mikono mifupi na iwe na mfuko mmoja tu upande wa kushoto, mikanda ya mabegani inayofanana na nguo za kijeshi hairuhusiwi.

iii) Viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi.

iv) Soksi nyeupe ndefu ***(stocking)*** pea tatu kwa ajili ya matumizi ya kila siku za shule.

v) Raba za michezo rangi yoyote na sare za michezo ***"jezi***" rangi ya bluu kwa ajili ya matumizi kwa siku za michezo tu na siyo darasani.

vi) Sweta rangi ya damu ya mzee isiyo na mistari myeupe shingoni na mikononi.

vii) T-shirt rangi ya zambarau yenye kola, kwa wanafunzi wa kiislam washone ***Hijabu*** ya zambarau.

b) Wavulana;

i) Suruali mbili rangi ya ugoro-udongo zilizoshonwa vizuri kwa kuzingatia taratibu, suruali za kubana('modo/kamatia chini') na kubwa zenye kuashiria kutepeshwa/mlegezo ni marufuku shuleni.

ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi kitambaa cha tetroni na iwe na mfuko mmoja kushoto isiyo na mifuniko wala mikanda ya kijeshi mabegani.

iii) Viatu vya ngozi vyeusi vya kawaida vya kufunga kwa kamba na siyo buti.

iv) Soksi nyeusi fupi pea tatu kwa matumizi ya kila siku za shule.

v) Raba za michezo rangi yoyote na sare za michezo "jezi" rangi ya bluu kwa ajili ya matumizi kwa siku za michezo tu na siyo darasani.

vi) Sweta rangi ya damu yam zee isiyo na mistari myeupe shingoni na mikononi.

vii) T-shirt rangi ya zambarau yenye kola.

VIFAA VYA DARASANI

i) Madaftari yasiyopungua 15 (counter book quire3) au madaftari ya msomi yaliyo unganishwa matatumatu.
ii) Kalamu 5 za wino na 3 za risasi.
iii) "Mathematical Set" 1.
iv) Mfuko wa kubebea vitabu na daftari (School Bag)
v) Rula 1.

VIFAA

i) Jembe 1 lenye mpini na mfagio mmoja wa chelewa kwa ajili ya usafi wa mazigira na kilimo.

BIMA YA AFYA

Mwanafunzi anatakiwa kuja na kiasi cha fedha Tshs 5,000/= kwa ajili ya Bima ya afya kama hana, mtoa huduma hiyo atakuwepo kwa ajili ya kutoa vitambulisho.

ZINGATIA:

i) Mzazi tafadhali siku ya kuripoti ongozana na mwanao shuleni ili kufanya makabidhiano mazuri na kamwe mwanafunzi asiripoti peke yake bila mzazi/mlezi.
ii) Mavazi yasiyo na heshima kama vile ya kubana sana na yaliyoshonwa kinyume na taratibu hayataruhusiwa kamwe, aidha sare ya shule hairuhusiwi kuvaliwa na nguo,vazi au kitu chochote ambacho si sare shule *Mfano* ***mikufu,pete au mapambo yoyote***.
iii) Mwandalie mwanao kila kitu kipya epuka kununua vitu kwa mwanafunzi aliyemaliza au anayendelea na masomo hasa ***sare za shule.***
iv) Fomu hii ya kujiunga inatakiwa kurudi shuleni ikiwa kwenye folder file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mwanafunzi.

3.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya taifa.
h) Kuwa mjamzito au kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na shelia kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

MTURI DANIEL
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SEEKE
KAHAMA-SHINYANGA

MAELEZO BAYANA (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

1. Jina kamili la mwanafunzi……..
2. Tarehe ya kuzaliwa; …….
3. Jina la baba/Mlezi ……
4. Jina la mama/Mlezi ……..
5. Kazi afanyazo baba …….
6. Kazi ya baba/mama …….
7. Anuani ya baba/mama …….
8. Ana kilema chochote ……...
9. Anapendelea kushiriki michezo gani……

10. Taja ndugu wasiopungua watano wa karibu, wanaoweza kutoa msaada kwa mwanao:-

S/Na.	JINA	UHUSIANO	KAZI	SIMU/ANUANI

FOMU YA MKATABA WA KUJIUNGA NA SHULE

I. Mimi……..Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi……..leo hii tarehe……nimeyaona na kuyaelewa maagizo na maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Seeke.Naapa/siapi kuyatekeleza maagizo yote ya shule kabla ya kumleta mwanafunzi na endapo nitashindwa kutimiza nitakuwa nimekiuka taratibu na maagizo aliyopewa mwanangu.

Naahidi/siahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa shule katika kumlea kijana wetu endapo kijana atakuwa amekiuka sheria.

Nakubaliana/sikubaliani na maagizo yote ya kujiunga na shule hii.

Saini ya Mzazi:……..Tarehe……

Namba ya simu:……..

II. Mimi…….(Mwanafunzi) nimeyasoma na kuyaelewa maagizo yote ya kujiunga na shule pamoja na sheria na kanuni za shule.

Nakubali/sikubali kufuata na kutii sheria zote za shule.

Jina la Mwanafunzi:…….....Saini……..

Tarehe:…….

PRESIDENTS OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MEDICAL EXAMINATION FORM

FROM: SEEKE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 1021
KAHAMA

TO

The Medical Officers

……

……

Please Examine the student called…….And indicate if he/she is fit/not to join/continue with studies.

1. Blood test……...
2. Chest……..
3. Eyes……
4. Asthma……...
5. TB-Test……..
6. Typhoid……
7. Pregnancy for female……
8. Operation……
9. Ears……
10. Others…….

…….
Signature and stamp of Medical Officer